CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

MAHAFALI YA ISHIRINI NA MOJA (21) KAMPASI YA KIVUKONI, MAHAFALI YA KUMI NA MOJA (11) KAMPASI YA KARUME - ZANZIBAR NA MAHAFALI YA NNE (4) KAMPASI YA PEMBA KWA MWAKA 2026

Mkuu wa Chuo anawatangazia wanafunzi waliohitimu masomo yao katika mwaka wa masomo 2025/2026 kwamba Mahafali katika kampasi zake zote tatu yatafanyika kama ifuatavyo; Kampasi ya **Kivukoni jijini Dar es salaam** ambayo ni **Mahafali ya ISHIRINI NA MOJA** yatafanyika siku ya **Ijumaa tarehe 20 Novemba 2026,** Kampasi ya **Karume visiwani Zanzibar** ambayo ni **Mahafali ya KUMI NA MOJA** yatafanyika siku ya Jumatatu tarehe 23 Novemba, 2026 **na kwa Kampasi ya Pemba ambayo ni Mahafali ya NNE** yatafanyika **siku ya Jumanne tarehe 24 NOVEMBA 2026. Mahafali YATAANZA SAA TATU ASUBUHI KWA KAMPASI ZOTE.**

Wahitimu wa Kampasi zote wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1 Kuchukua Majoho kwa Kampasi ya Kivukoni ni kuanzia **Jumatatu, tarehe 16.11.2026 hadi Alhamis Novemba, 19 2026,** kwenye ofisi namba 115 – Jengo la Uhuru, **Kampasi ya Karume - Zanzibar majoho yatatolewa kuanzia siku ya Jumamosi tarehe 21 Novemba 2026 hadi siku ya Jumapili ya tarehe 22 Novemba 2026, na Kwa Kampasi ya Pemba Majoho yatatolewa tarehe 23 siku ya Jumatatu Novemba 2026.**

Majoho kwa kampasi zote yatatolewa kuanzia **4:00 asubuhi hadi saa 9:00 Alasiri,** na kuwa **Majoho hayatatolewa siku ya mahafali.**

2. **MALIPO YOTE YA KULIPIA MAJOHO YALIPWE KWA KUTUMIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI (CONTROL NUMBER)**

3. Majoho sharti yarejeshwe Chuoni kabla ya **tarehe 27 Novemba, 2026 kwa Kampasi zote.** Vinginevyo **faini ya shilingi 10,000/=** itatozwa kwa siku kwa yeyote atakayechelewa kurudisha joho hilo.

4. kusanyiko la wahitimu wote yaani **(CONVOCATION)** waliosoma katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere litafanyika katika Kampasi ya Kivukoni jijini Dar es Salaam siku ya **Alhamis, tarehe 19 Novemba 2026** katika Ukumbi mpya wa Mihadhara **(NEW LT**) chuoni hapo kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa sita mchana.

5. Zoezi la namna ya kupokea vyeti **(REHEARSAL**) kwa kampasi ya Kivukoni litafanyika **Alhamis, tarehe 19 Novemba, 2026** kuanzia **saa 6.00 mchana** na mahafali yatafanyika katika uwanja wa Mpira **Kampasi ya Kivukoni. Kampasi ya Karume-Zanzibar** zoezi hilo

litafanyika **tarehe 22 Novemba siku ya Jumapili 2026** kuanzia **saa 4:00 asubuhi** katika uwanja wa mahafali Chuoni hapo, Na kwa **Kampasi ya Pemba rehearsal** itafanyika siku ya Jumatatu tarehe 23 Novemba 2026 katika viwanja vya Kampasi ya Pemba Pujin, Chakechake Pemba.

Mhitimu atakayeshindwa kuhudhuria zoezi hilo la REHEARSAL HATARUHUSIWA kushiriki katika Mahafali.

6. Kila mhitimu atapaswa kujigharamia usafiri, malazi na chakula.

7. **WASHIRIKI WOTE WA MAHAFALI WANATAKIWA KUTHIBITISHA USHIRIKI WAO KATIKA OFISI YA MITIHANI KABLA YA tarehe 17 Novemba, 2026 kwa kupiga simu namba zifuatazo: 0679907412, 0782405552 na 0762020129**

NYOTE MNAKARIBISHWA.

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,
S.L.P. 9193,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2820041/ 2820045/ 2820047
Faksi: +255 22 2820816
Barua pepe: rector@mnma.ac.tz